



Kuku na Jongoo



- ✍ Winny Asara
- ✎ Magriet Brink
- ☞ Matteo E. Mwita
- 💬 swahili
- 🔊 nivå 3



Kuku na Jongoo walikuwa marafiki. Ila walikuwa wanashindana kila mara. Siku moja wakaamua kucheza mpira wa miguu ili waweze kubaini nani alikuwa mchezaji bora zaidi.




Wakaenda uwanjani na wakaanza kucheza. Kuku alikuwa na kasi ila Jongoo alikuwa na kasi zaidi. Kuku alipiga mpira mbali, ila Jongoo alipiga mbali zaidi. Kuku akaanza kupandwa na hasira.




Wakaamua kupigiana penati. Jongoo akaenda golini. Kuku alifunga goli moja pekee. Ikawa zamu ya kuku kwenda golini.

Jongoo alipiga mpira akafunga. Jongoo akapiga chenga akafunga. Jongoo akapiga kichwa akafunga. Jongoo akafunga magoli matano.






Kuku akakasirika kwa kuwa amefungwa. Hakuwa mshindani mzuri. Jongoo akaanza kucheka kwa sababu rafiki yake alikuwa analalamika.



Kuku alipatwa na hasira kiasi kwamba akafungua
mdomo wake mkubwa na akammeza Jongoo.



Kuku alipokuwa anarudi nyumbani alikutana na Mama yake Jongoo. Mama Jongoo akamuuliza, "Umemwona mwanangu?" Kuku hakujibu kitu. Mama Jongoo akapatwa na wasiwasi.



Mama Jongoo akasikia sauti kwa mbali. "Nisaidie mama!" ile sauti ililia. Mama Jongoo akaangalia huku na kule na kusikiliza kwa makini. Sauti ilitokea tumboni mwa kuku.



Mama Jongoo alipiga kelele, "Tumia nguvu yako ya kipekee mwanangu!" Majongoo wanaweza kutoa harufu mbaya na ladha ya ajabu. Kuku akaanza kujisikia mgonjwa.



Kuku akabeuwa. Akameza mate na kutema.
Halafu akapiga chafya na kukohoa. Akakohoa
tena. Jongoo alimfanya ajisikie vibaya.



Kuku alikohoa, hadi akamtema jongoo aliyekuwa tumboni mwake. Mama Jongoo na mwanaye wakakwea mti kujificha.



Tangu hapo, Kuku na Jongoo ni maadui.



Barnebøker for Norge

barneboker.no

Kuku na Jongoo

Skrevet av: Winny Asara

Illustrert av: Magriet Brink

Oversatt av: Matteo E. Mwita

Denne fortellingen kommer fra African Storybook (africanstorybook.org) og er videreført av Barnebøker for Norge (barneboker.no), som tilbyr barnebøker på mange språk som snakkes i Norge.

Dette verket er lisensiert under en Creative Commons
[Navngivelse 3.0 Internasjonal Lisens](#).